MUNGU NDIYE ANAYEJIFASIRIA

Baba yetu wa Mbinguni, Neno moja kutoka Kwako lingekuwa na maana zaidi kuliko yote mwanadamu wakati wo wote angeweza kufanya au kusema, kwa sababu watu wanangojea kukuona Wewe. Nasi tunakushukuru Wewe kwa sababu kuna wale ambao wako kwenye matazamio, wanatazamia jambo fulani litukie. Na wakati watu wanasikia kiu ya jambo fulani, kilindi kikiita Kilindi, lazima kuwe na Kilindi cha kuitikia mwito huo. Na hiyo ndiyo sababu tupo hapa usiku wa leo, kwa sababu ni kitu kilikuwa katika mioyo ya wahudumu hawa, na watu, kutuita pamoja kukuomba Wewe msaada na baraka, tukiamini kwamba utawaponya wagonjwa na kuwaokoa waliopotea, na utadhihirisha Neno Lako.

2 Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utatukirimia hili tukikungojea kwa unyenyekevu, usiku baada ya usiku. Jalia kuwe na—na kushuka kwa Roho Mtakatifu, na hebu kila mtu awe kipofu kwa kingine cho chote kinachowazunguka ila Mungu. Na kitoke kilio kikuu miongoni mwa watu, wakimwonea Mungu kiu, mpaka kuje uamsho nchini pote hapa na kila kanisa lijae watu, wenye dhambi wakimlilia Mungu wapate rehema, na—na Roho Mtakatifu akiponya wagonjwa, akawafanya viwete watembee, na kufufua wafu, na kutukirimu mambo haya ambayo yameahidiwa katika Neno Lako.

3 Njoo, Bwana Yesu, utimize ahadi Yako. Njoo kwetu usiku huu. Tunaamini kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo na hata milele, kwamba ahadi Zako haziwezi kushindwa. Mbingu na nchi zitashindwa lakini Neno Lako halitashindwa. Hebu ufahamu wetu na ufunguke. Roho Mtakatifu na aje aandae shamba. Ufahamu wetu na ufunguke kwa Roho na nguvu za Mungu usiku huu, ili Yeye aweze kudhihirisha Maneno Yake ya ahadi kupitia kwetu. Kwa kuwa tunaomba hivi katika Jina la Yesu. Amina.

4 Sasa, usiku wa leo, ninyi mnaoangalia kifungu, tufungue Biblia kwenye Kitabu cha 2 Petro, na kuanzia na aya ya 15, kwa namna tu ya kuzungumzia juu ya Andiko kwa muda mchache.

> *Walakini nitajitahidi, kwamba wakati baada ya kufariki kwangu tupate kuyakumbuka mambo haya.*
>
> *Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake.*

5 Napenda hilo, "tumeuona wenyewe." Si hadithi zilizotungwa. Tu mashahidi wa yale tunayoyazungumzia.

Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika utukufu mkuu; Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.

Na sauti hiyo sisi tuliisikia ikitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika mlima ule mtakatifu.

Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'arayo. . .mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.

Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.

Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

6 Bwana na aongezee baraka Zake kwenye usomaji wa Neno Lake. Sasa, naenda kuchukua hili kwa ajili ya somo: *Mungu Ndiye Anayejifasiria.*

7 Tunaishi katika siku ya machafuko. Tunaishi katika siku ambayo ni wakati ambapo mwanamume na mwanamke ni vigumu sana kujua la kufanya. Kila kitu, ki—kinaonekana kuwa katika vurugu. Kila kitu, inaonekana kuwa kuna njia nyingi sana za kutazama. Huyo ni Shetani, kufanya jambo hilo.

8 Sasa, Mungu hawezi kuhukumu watu kwa haki, sawasawa, isipokuwa kuwepo na kipimo fulani ambacho kwa hicho Yeye itampasa kuwahukumu. Na Biblia husema kwamba Yeye atawahukumu watu wote kwa Yesu Kristo, na Yesu Kristo ni Neno. Katika Mt. Yohana, sura ya 1, linasema:

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, . . .

9 Sasa, namna zote tulivyo leo ni maonyesho ya sifa Zake. Katika Mungu. . .Kwanza Yeye hata hakuwa Mungu, Mungu, tungemwita tu "Yule wa Milele." Yeye hakuwa Mungu, kwa sababu neno (neno la Kiingereza) *Mungu* humaanisha "kitu cha kuabudiwa" na hapakuwepo na kitu cha kumwabudu Yeye. Kwa hiyo Yeye alikuwa Ndiye Wa Milele, ile—ile Chemchemi kuu ya ufahamu wote. Na katika Chemchemi hii ya ufahamu wote hapakuwepo na hata atomi, chembe ndogo sana, cho chote, nuru haikuwapo, nyota, mwezi, au cho chote kingine. Mungu, yule tumjuaye kama Mungu, yule Roho Mkuu aliyekuwa wa Milele (kamwe hakuanza, kamwe hakuwa na mwisho), Yeye alikuwepo. Na katika Yeye mlikuwepo sifa: ilikuwa sifa za kuwa Mungu, kisha sifa Zake kuwa Baba, sifa kuwa Mwana, sifa kuwa Mwokozi, sifa kuwa Mponyaji. Sifa zote hizi zilikuwa katika

Yeye. Na sasa Yeye . . . mambo haya ambayo yamefunuliwa tangu hapo ni sifa Zake tu zikiwa zinadhihirishwa.

10 Ninalomaanisha, *sifa*, zilikuwa "mawazo" Yake. Na ne—*neno* ni "wazo lililotamkwa." Na basi hilo lilikuwa katika wazo Lake. Na Yeye aliposema, "Iwe," ikawa. "Iwe," ikawa.

11 Na sasa, kumbukeni, ninyi Wakristo mlikuwa mawazo Yake kabla ya kuwepo ulimwengu. Nanyi ni udhihirisho wa mawazo Yake. Kabla ya hata kuwepo na ulimwengu, ninyi mlikuwa katika Kristo, (amina) katika Mungu mwanzoni. Hilo huwafanya nyinyi basi, mnaona, raia Wake. Na jambo lote zima ni Mungu, Mwenyewe, akijitokeza Mwenyewe katika umbo ligusikalo ili Yeye aweze kushikika, kuonekana, na—na kadhalika. Na hivyo ndivyo Mungu alivyo, jambo lote zima.

12 Ndipo watu husema, "Tafsiri . . . " Nilikuwa nikizungumza hapa si muda mrefu uliopita katika mkutano, mtu mmoja akaniambia, akasema, "Ndugu Branham, una tafsiri mbaya. Hutafsiri Hilo kwa usahihi."

13 Sasa, tunasikia . . . Wao huenda kwa Wamethodisti, nao husema "Wabatisti hawafasiri sawasawa." Wabatisti wanasema, "Wapentekoste hawafasiri sahihi." Wapentekoste husema kwamba "Wa—wa Umoja hawafasiri sahihi." Wa Umoja husema, "Waasembly hawafasiri sawasawa." Na kila mmoja husema mwenziwe hafasiri sahihi.

14 Mungu Ndiye anayejifasiria! Hahitaji mtu ye yote amfasirie. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Ni mtu gani ambaye anaweza kumfasiri Mungu? Mungu hujifasiria Mwenyewe.

15 Sasa, Petro akinena hapa, tunaona kwamba hapo mwanzo Mungu aliposema, "Iwe nuru," na nuru ikawepo, hiyo ndiyo tafsiri yake. Mungu aliponena kitu cho chote na kikadhihirishwa, basi hiyo ndiyo tafsiri ya Mungu kwamba Neno Lake ni kweli. Unaona? Wakati Yeye aliposema, "Iwe nuru," hilo lilikuwa mawazoni Mwake kwanza kabla ya kuwepo kitu kama nuru. Yeye aliposema, "Iwe nuru," nuru ilitokea kule angani, hiyo ndiyo tafsiri. Hakuna mtu apaswaye kufasiri hilo, kwani Mungu alinena hivyo na hapo ikatokea. Mungu anenapo na inadhihirishwa, hiyo ndiyo tafsiri ya Neno Lake. Kwa nini binadamu asione hilo? Kwa nini watu wasione hilo?

16 Mungu anapoahidi kitu na Mungu anasema . . . Hapo—hapo mwanzo, katika Mwanzo, alipanga Neno Lake kwa kila wakati lilipokuja toka mwanzoni hadi mwisho. Na, kupitia nyakati hizi, ulimwengu wa kanisa lomeyachanganya mambo yote haya kwa mapokeo, na kadhalika, na Mungu sikuzote huwapeleka, katika Agano la Kale na Jipya, manabii! Na Neno la Bwana humjia nabii. Na linafanyaje? Hudhihirisha Neno la Mungu. Udhihirisho wa Mungu, huo huonyesha kama ni sahihi au si sahihi. Hakuna mtu anayepaswa kulifasiri, Neno hujifasiri Lenyewe. Mungu aliliahidi na hapo linatukia!

17 Yafaa nini kunena kitu cho chote kingine juu ya hilo? Mtu yupi mwenye dhambi ambaye angejaribu kusema (wakati Mungu ameahidi kitu na Mungu anakifanya) kwamba tafsiri hiyo si sahihi? Huyo ni Mungu Mwenyewe akitoa tafsiri Yake Yeye Mwenyewe, akifasiri. Hahitaji mtu ye yote kumfasiria, Yeye hujifasiria Mwenyewe kwa kudhihirisha aliloahidi kwamba angetenda.

18 Loo, laiti kanisa lingeweza kuona hilo na kuona zile ahadi ambazo zimepangwa kwa kila wakati! Nyakati nyingine zote, Mungu amepeleka (hata katika zile nyakati saba za kanisa) na amedhihirisha kila kitu ambacho aliahidi kufanya. Kila kitu, hakuna hata kitu kimoja ambacho hakikufanywa. Sawa kabisa! Alilosema angetenda, hilo alitenda.

19 Kwa sababu Mungu aliposema, nyuma huko katika Isaya, alisema, "Bikira atachukua mimba," na akachukua mimba. Sasa, nani—nani anaweza kufasiri hilo? Mungu alifasiri. Alisema, "Bikira atachukua mimba," na alichukua mimba. Sasa, wewe ni nani . . . huwezi . . . Hakuna cha kusema kuhusu hilo, kwa sababu Mungu alisema bikira angefanya hivyo naye akafanya. Lakini kanisa lilikuwa kipofu sana wakati huo kuona hilo. Unaona, walikuwa na mawazo yao wenyewe ya kitu hicho. Ilikuwa—ilikuwa tofauti sana na walilokuwa wakitazamia.

20 Petro hapa alikuwa akirejea nyuma, akasema, "Mungu alimdhihirisha Kristo kwa Neno Lake, alisema, 'Huyu ni Mwanangu mpendwa." Waamini hawa walikuwa wamesimama pale. Na Kristo alikuwa udhihirisho wa Mungu. Sikuzote humdhihirisha Kristo kwa Neno Lake, kwa sababu Kristo ni Neno. Hudhihirisha sikuzote.

21 Aliposema . . . Katika siku za Nuhu, Kristo alikuwa katika Nuhu. Unaamini hilo? Nuhu alisema, "Itanyesha. Kutakuwa na mvua, dunia itaangamizwa." Ilinyesha. Hilo halikuhitaji tafsiri yo yote. Ilinyesha kwa sababu Mungu, katika Nuhu, alisema, "Itanyesha." Alikuwa nabii, na dhihirisho lilikuwa kwamba alilosema lilitimia. Kwa hiyo hawahitaji kufasiri hilo.

22 Baadhi yao labda, waliokuwepo, walisema, "Mtu huyu hajui anachozungumzia."

23 Lakini sikuzote Mungu aliahidi, "Akiwepo mmoja kati yenu ambaye ni wa rohoni, au nabii, nalo anenalo linatimia, basi lisikilizeni." Hilo ni sawa, kwa sababu ni kweli. Lazima lipatane na Neno. Na Nuhu alipatana na Neno. Alipotabiri itanyesha, na ilinyesha. Hilo halikuhitaji tafsiri yo yote kwa hilo, kwa sababu alitendeka hivyo tu.

24 Isaya alisema, "Bikira atachukua mimba," naye alichukua mimba. Sasa, hilo lilikuwa si la kawaida kabisa. Kwa maana, unaona, ilikuwa miaka mia kadhaa baadaye kabla ya bikira huyu kuchukua mimba.

25 Lilikuwa lisilo la kawaida sana mpaka mtu mzuri jina lake Yusufu, mumewe, "alikuwa mtu mwenye haki naye hakutaka kumwaibisha . . . " Mtu huyo mzuri katika siku hizo, jinsi ilibidi kuwa kwa Yusufu hapo alipokuwa amemposa, amemposa Mariamu.

26 Alikuwa ameposwa. Katika siku hizo, kuvunja hilo, ilikuwa sawa tu na kuzini. Na, bila shaka, kwa Yusufu, ilionekana kana kwamba Mariamu alikuwa anajaribu kumtumia kama mazingiwa, au amfanye yeye kinga kwa kosa lake, sababu hapa alionekana kuwa na mimba, akiwa hajaolewa, alikuwa ameposwa tu. Ujanja kama huo, angeuwawa kwa kupigwa mawe; ilibidi iwe hivyo, kwa sheria.

27 Na Yusufu, mumewe, alikuwa mtu mwenye haki, mtu mwenye haki sana. Alimwamini Mungu. Na wakati alipomtazama Yusufu kwa macho hayo mazuri, macho makubwa na mororo, na kusema, "Yusufu, Malaika mkuu Gabrieli alinizuru na kuniambia kwamba nitachukua mimba, bila ya kumjua mwanamume."

28 Sasa, kama Yusufu angeangalia nyuma tu katika Maandiko, nabii alinena angefanya hilo. Ilikuwa Mungu tu akifasiri Neno Lake! Unaona? Lakini lilikuwa jambo geni mno.

29 Hiyo ndiyo shida katika wakati wo wote. Neno la Mungu ni geni kwa watu; ni la kushangaza mno. Mungu sikuzote kutenda yasiyo kawaida. Si kitu cha kawaida po pote Mungu alipo. Ni kinyume cha taratibu za ulimwengu, kwa sababu ya kwamba wanayatazamia mambo namna ambayo huyafikiria yangekuwa. Lakini Mungu huja na kutenda kisicho cha kawaida.

30 "Bikira huyu angewezaje kuchukua mimba?" Alikuwa mwaminifu, alimtaka Mungu shauri kuhusu hilo.

31 Na kisha Mungu alinena naye katika ndoto, na akasema, "Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Mungu alimfunika kama kivuli. Hili ndilo lililotenda hilo."

32 Uliangalia angalia jinsi Mungu alivyoshughulika na Yusufu hapo? Katika njia hafifu, katika njia ya ndoto. Sasa tunajua kuna ndoto, tunaamini ndoto. Ninaamini ndoto. Amekuwa . . . Mungu sikuzote ameshughulika na watu katika ndoto. Lakini ndoto ni njia hafifu, unaona, ingeweza kuwa sawa au kosa isipokuwa imefasiriwa. Lakini yeye hakuhitaji tafsiri yo yote. Ilikuwa Mungu Mwenyewe akimzungumzia Yusufu moja kwa moja, kwa sababu hapakuwepo na nabii nchini katika siku hizo kufasiri. Hapakuwepo na nabii kwa miaka mia nne. Kwa hiyo kitu cha pili kilichofaa sana, ambacho kwa hicho Mungu a—alimtunza Mwanawe, ilikuwa kuzungumza na Yusufu katika ndoto na bila ya kutafsiriwa. Alisema, "Huyo mwanamke yuko sahihi. Hicho Kitu Kitakatifu ambacho kimechukuliwa mimba ndani yake ni Mwana wa Mungu." Haikuhitaji tafsiri yo yote.

33 Mungu hufasiri Yeye Mwenyewe kwa mioyo miaminifu, mioyo minyofu, wanaume na wanawake ambao kuangalia ki—kitu ambacho ni cha ajabu, kama wewe ni mwaminifu na mnyofu na utaamini, Mungu anayo njia ya kukutafsiria hilo. Kwanza, chunguza kama ni ahadi. Kama Yusufu angerudi tu nyuma na kutoka kwenye mapokeo na kurudi kwenye Biblia, na kuchunguza, Isaya alisema huyo angefanya hilo.

34 Na yale mambo yaliyonenwa, na kuzaliwa Kwake, na yote yaliyohusu jambo hilo yalikuwa yamenenwa kwa Maandiko, "kwa manabii watakatifu," kama Petro alivyosema. Na hakuna mtu aliye na haki ya kuweka tafsiri yake mwenyewe ya hilo. Ni kile tu hasa Mungu alisema kitatukia. Alikuwa udhihirisho wa Neno la Mungu lililoahidiwa kwa siku ile. Mungu alilinena, kwa hiyo hapo likawa. Hilo lilimaliza mambo yote.

35 Yesu alisema . . . Alipokuwa duniani, wakati waliposhindwa kuelewa huduma Yake, ilikuwa kubwa mno, ya ajabu sana, (hawakuweza), ya ajabu, hasa. Hawakuweza kumwelewa. Alisema, "Yachunguzeni Maandiko!" (Natumaini siyashindi masikio yenu huko, nikiwapigia makelele hivyo.) "Mwachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake, na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Unaona? "Ndiyo yanayowaambia Mimi ni Nani."

36 Unaona, Mungu aliligawa Neno. Wakati huo ulikuwa wa kudhihirishwa kwa Mungu, Mungu (Imanueli) pamoja nasi, "Jina Lake ataitwa Wa Ajabu, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele. Na Jina Lake ataitwa *Imanueli*, 'Mungu pamoja nasi.'" Mungu alikuwa katika Daudi. Mungu alikuwa katika Musa. Mungu! Huyo alikuwa ni Mungu wakati wote, akijidhihirisha Mwenyewe kwa wakati ule. Lakini wakati huu, "Bikira atachukua mimba naye atazaa mwana, naye atakuwa Mungu pamoja nasi."

37 Hilo ndilo walilomsulubishia, kujifanya Mwenyewe Mungu, na pia kwa kuivunja Sabato. Yeye alikuwa—alikuwa Mungu juu ya Sabato, naye alikuwa Mungu. Naye hakuwa tu mtu wa kawaida au nabii wa kawaida (hata hivyo Yeye alikuwa Mtu wa kawaida na Nabii), lakini alikuwa Mungu-Nabii. Na alikuwa utimilifu wa Neno, vile kabisa ambavyo Mungu alisema angefanya. Alisema, "Ni yupi miongoni mwenu anishuhudiaye nina dhambi? Yachunguzeni Maandiko! Ndani yake ninyi mnadhani mna Uzima wa Milele, na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Lakini mapokeo yao, walikuwa wakiishi katika mng'aro wa wakati mwingine.

38 Kama nilivyokuwa ninahubiri majuma machache yaliyopita, *"Kuishi katika mng'aro." Mng'aro* ni "mazigazi," jua likirudisha nuru yake lenyewe, na ni kitu cha uongo. Na mng'aro wo wote wa wakati mwingine ni nuru ya uongo. Watu sikuzote wanatembea katika kitu ambacho kimetokea miaka mingi iliyopita. Waluteri

wanatembea katika mng'aro wa Kiluteri. Nuru ya jua ya Luther ilikuwa nzuri katika siku yake; Wesley alikuwa mzuri katika siku yake; Upentekoste ulikuwa unafaa katika siku yake. Tunakwea ngazi, tunaishi katika wakati mwingine! Tunaendelea, kuendelea, hatuwezi kuendelea kutazama nyuma.

39 Tunapotulia katika mambo fulani, tunafikiri kila kitu tumekiweka sawa, tunafungafunga desturi zetu; na hilo lilikuwa sawa kwa siku hiyo, lakini tunapiga hatua! Yachunguzeni Maandiko muone ambalo limeahidiwa kwa wakati wa leo, ndipo tutakapojua ni wapi tulipo, ndipo tunaweza kujua tunasimama wapi.

40 Luther; ungeweza kuangalia katika Maandiko na kuona katika hayo—katika ule wakati wa Sardis, unaweza kuona sawasawa kilichokuwa kimeahidiwa. Angalia ni mpanda farasi wa namna gani alitoka, angalia ambacho kilitoka kwenda kukabiliana naye, sawa kabisa, "werevu wa mwanadamu," na yale Matengenezo. Mwangalie Wesley, na kadhalika. Wakati inakuja kwenye wakati wa Upentekoste, na kupitia wakati ule, angalia jinsi lilivyoenda. Angalia Maandiko uone tulipo. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, "Yachunguzeni maandiko!"

41 Angalieni tulipo! Naamini tuko katika wakati wa Kuja kwa Mwana wa Mungu sasa hivi. Naamini tupo wakati wa—saa hasa ambayo anaweza atokee wakati wo wote. Naamini Maandiko yanatangaza hilo, kwamba tupo katika saa za mwisho za historia ya ulimwengu huu. Naweza kuona mambo yanavyoendelea. Kuona hii Halmashauri ya Ukomeni ikiyaongoza makanisa yote kwake, kwenye ile Alama ya Mnyama. Na kuona Milki ya Kirumi na ambalo inatenda, na wengine wote waliobakia. Kuwaona wakikusanyika pamoja, wakiifungia Nuru nje, wakiifungia nje Injili. Kila mtu itambidi awe wa hiyo na atembee katika nuru zao ama sivyo hutatembea hata kidogo. Unaona, tumefikia wakati wa mwisho. Hakuna kilichobakia kwetu bali kumshikilia Mungu na kuliamini Neno Lake. Neno sikuzote ni sahihi.

42 Katika wakati wa kanisa wa Laodikia, huo ndio uliokuwa wakati wa kanisa pekee, miongoni mwa zote, ambapo Kristo alikuwa amewekwa nje ya kanisa. Alikuwa nje, akibisha. Nini kimetukia? Halmashauri hii ya Ekumeni ndiyo itakayomtoa nje. Biblia ilisema angekuwa nje, na yuko nje. Inafungia nje nini? Neno. Na Yeye ni Neno, sikuzote amekuwa Neno, na bado Yeye ni Neno usiku wa leo! Yeye ni Neno.

43 Biblia ilisema, "Neno lina ukali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili." Waebrania, sura ya 4, "huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Neno lilikuwa! Walipaswa kujua Yeye alikuwa nani wakati Yesu aliponena hilo katika siku hiyo.

44 Angalieni alilofanya. Siku moja alikuwa amesimama pale, mwanzo kabisa wa huduma Yake. Palikuwa na mtu aliyemjia, kwa jina la Simoni, Simoni Petro. Na Petro alipomtazama na—na

akamwona, Yesu alimwambia, “Jina lako ni Simoni na u mwana wa Yona.” (Angepaswa kujua kwamba Musa alisema, “Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii kama nilivyo mimi, na hamna budi kumsikiliza Yeye.” Na hapa alikuweko mtu ambaye kamwe hajamwona katika maisha yake, akasema, “Jina lako ni Simoni nawe u mwana wa Yona.” Mbona, alijua papo hapo kwamba hilo haliwezi tena kuwa. . .Hawajawa na nabii kwa mamia ya miaka, na hapo yupo mtu aliyemwambia yeye ni nani. Si ajabu aliweza kupokea hilo!

45 Filipo, wakati huo alikwenda na—na akamkuta Nathanieli chini ya mti, naye akamleta kwa Yesu. Yesu akasema, “Tazama Mwisraeli, hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Rabi, umepataje kunitambua?”

46 Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.”

47 Akasema, “Rabi, wewe u Mwana wa Mungu! Ndiwe Mfalme wa Israeli.” Alijua huyo alikuwa! Nini? Haikuhitaji tafsiri yo yote, Yehova alinena hilo!

48 Palisimama wale pale ambao hawakuliamini. Walisema, “Mtu huyu ni Beelzebuli. Ana—ana namna fulani ya ujanja anaoufanya. Yeye—Yeye ni mpiga ramli, au kitu fulani.”

49 Yesu aliwatazama, na akasema, “Mbona, mkinena hilo dhidi ya Mwana wa Adamu, mtasamehewa. Lakini Roho Mtakatifu ajapo kutenda kitu hicho hicho, kunena dhidi ya Hilo, hamtasamehewa kamwe jambo hilo katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Alikuwa anatabiria siku zetu, siku ambazo tungeona. Kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Kumbuka, ilikuwa Yesu Kristo ambaye alikuwa ndani ya Musa.

50 Ilikuwa Yesu Kristo ambaye alikuwa katika Daudi. Wakati Daudi, mwana wa. . .Daudi alipanda mlimani, mfalme aliyekataliwa, naye akaulilia Yerusalemu, huyu si mwingine bali ni Kristo ndani yake. Kwa kuwa yapata miaka mia nne baadaye, Mwana wa Daudi aliketi juu ya Mlima wa Mizeituni akautazama Yerusalemu akalia, kisha akasema, “Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake, lakini hamkutaka!”

51 Yusufu alipokuwa jela, huyo alikuwa ni Yesu. Alipouzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha, huyo alikuwa Yesu. Alipofanywa mtu wa Potifa, huyo alikuwa Yesu. Alipoketi mkono wa kuume wa Farao. Na alipoondoka, kila mtu. . . tarumbeta ililia, na kila mmoja ilimlazimu kupiga goti, huyo alikuwa Yesu. Hakuna mtu aliyeweza kuja kwa Farao isipokuwa kwa kupitia—kwa kupitia kwa Yusufu; hakuna mtu awezaye

kuja kupitia Mungu isipokuwa kwa Yesu. Ilikuwa Yesu, Neno lililotabiriwa likitimilizwa, lilinenwa katika vivuli na mifano.

52 Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani alitenda jambo lile lile manabii walilotenda, hiyo ndiyo sababu walijua kwamba alikuwa udhihirisho wa Mungu wa Neno Lake. Halikuhitaji kufasiriwa.

53 Wakati Nathanieli alipoona hili, alianguka chini, akasema, "Wewe ni Mfalme wa Israeli, Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli. Tunakujua, hakuna mtu angeweza kutenda hili."

54 Nikodemo akaja usiku, akasema jambo lile lile kwa Mafarisayo. Lakini, unaona, walikuwa wameshikwa sana katika Halmashauri yao ya Ekumeni hata hawakuweza kulikubali. Alielezea walilosema, kasema, "Rabbi, sisi . . . " "Sisi" ni nani? Halmashauri yao! "Twajua ya kwamba Wewe ni mwalimu unayetoka kwa Mungu, kwa sababu hakuna mtu angeweza kufanya mambo haya isipokuwa Mungu awe pamoja naye." Walitambua hilo, walijua ilikuwa hivyo, lakini walikuwa wameshikwa sana nalo.

55 Na Mungu, katika miaka arobaini iliyopita, ametikisa taifa hili kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, na mwanamume na wanawake bado wako nje yake kwa sababu wameshikwa katika kitu kile kile, wakiishi katika mng'aro wa siku nyingine. Kuna nini? Kila mmoja anapenda kuwa Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteria, Mluteri, au kitu fulani. Unaona, ni mng'aro.

56 Walikuwa wakiishi katika mng'aro wa siku ya Musa. Alisema nini? Alisema . . . Walisema, "Sisi tu wanafunzi wa Musa."

57 Akasema, "Kama mngemjua Musa, mngenijua Mimi. Musa aliandika habari Zangu!"

58 Kama mngemjua Luther mngefahamu wakati huu! Kama mngefahamu Methodisti, mngefahamu wakati huu! Kwa maana Kristo aliandika habari za wakati huu! Maneno ambayo yanatimilizwa yapaswa kutimilizwa katika wakati huu. Haihitaji mtu kuifasiri, Mungu hujifasiri Yeye Mwenyewe. Mungu hujifasiria Mwenyewe, kwa sababu ndiye pekee ambaye anaweza kufasiri Hilo. Ahadi za Mungu sikuzote huthibitisha ambalo alisema Yeye, na hiyo ndiyo tafsiri.

59 Sasa, Yesu, (kuokoa wakati), Yesu alisema, katika Yohana Mt. sura ya 14, aya ya 12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya." Je! alilisema? Hilo ni sawa. Hilo halihitaji kufasiriwa kwokwote. Mtu atendapo kazi hiyo, huyo ni Mungu. Bila shaka!

60 Pia alisema hapo, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Yesu alisema hilo. Je! Alilinena hilo? Hakika, alilinena! Hilo halihitaji kufasiriwa.

Wanasema, "Vema, hilo lilimaanisha . . . "

61 Lilimaanisha kabisa kile Yeye alichosema! “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, hivyo ndivyo itakavyokuwa ajapo Mwana wa Adamu.” Vipi siku za Lutu? Hebu turudi nyuma kidogo tu, tuone walichokuwa wakifanya.

62 Kulikuwa na watu wa tabaka tatu katika siku za Lutu: mwamini, mwamini wa kujifanya, na asiyeamini. Hilo lipo katika kila kundi, jambo lile lile.

Twaona kwamba Msodoma alikuwa asiyeamini.

Lutu alikuwa mwamini wa kujifanya.

63 Ibrahimu alikuwa mwamini. Ndiye ambaye agano lilithibitishwa kwake. Ndiye aliyekuwa anatazamia mwana wa ahadi. Ndiye aliyekuwa anamtazamia. Amina. (Mimi sijisemei “amina” mimi mwenyewe. *Amina* maana yake ni “Na iwe hivyo!”) Na hilo ni sawa. Ibrahimu hakuwa Sodoma. Ibrahimu alikuwa juu na nje ya Sodoma. Yeye ni mfano wa Kanisa la kiroho leo.

64 Lutu ni mfano wa kanisa la kidhehebu lililoko kule chini katika Sodoma bado. Angalia, Biblia ilisema kwamba, “Dhambi za Sodoma ziliitesa roho yake yenye haki kila siku.” Kwa nini hakuthubutu kuzipinga? Wapo watu wengi wazuri wanaoketi kanisani leo, wanaowaona wanawake wamevaa kaptura na wanaume wakifanya mambo haya, na wafuasi wao wakienda, wakicheza mpira wa ving’oe Jumapili, na karamu za mandari, na kuogelea na mambo, badala ya kuhudhuria kanisa. Wakikaa nyumbani Jumatano usiku, wakiangalia televisheni, badala ya kuhudhuria kanisa. Wanajihisi kusema kitu kuhusu hilo, lakini halmashauri itawatupa nje. Kuna nini? Ni Lutu tena, akiangalia kwenye dirisha lake na kuona hiyo dhambi, na kuogopa kuita dhambi “dhambi”!

65 Ibrahimu hakuwa katika vurugu yao, alikuwa nje yake. Alikuwa mfano wa Kanisa la kiroho. Sasa hebu angalieni tu lilitukia mwishoni mwa wakati, kabla tu ya moto kuanguka. Na hao walikuwa watu wa Mataifa. Ilionyesha kivuli cha moto ukivangukia ulimwengu wa Kimataifa leo. Wakati falme zitakapovunjika na zitaunguzwa. “Mbingu zitashika moto,” asema Bwana, “nazo zitateketezwa.” Hicho kilikuwa kivuli chake.

66 Sasa hebu tuwapige picha. Ibrahimu yuko hapa tayari ameishatoka, hayupo Sodoma, alikuwa nje ya Sodoma. Lutu bado alikuwa Sodoma.

67 Jambo la ajabu, asubuhi hiyo moja yenye joto, lazima ilikuwa mnamo saa tano, aliona watu watatu wanakuja, watu wa kawaida, wanatembea barabarani, kinjia. Ibrahimu alikuwa ameketi chini ya mwaloni, amestarehe. Alikuwa ametoka, labda pamoja na mifugo asubuhi ile, akaingia, yapata adhuhuri. Naye aliona watu watatu wanakuja. Na kulikuwa na kitu fulani juu ya hao watu, ambacho, kilipiga kengele. Loo, jamani!

68 Sikuzote kuna kitu fulani kuhusu Mungu, wakati kinapokuja miongoni mwa watu, hupiga kengele. Wao hujua hilo. Kuna kitu kinachowaambia, kuna thibitisho fulani hapo.

69 Ibrahimu aliendа mbio, na akasema, "Bwana wangu, karibu na naomba niwaletee maji kidogo, myachukue mkanawe miguu, na niwape chakula kidogo, baadaye muendelee na safari yenu." Kwa hiyo akageuka. Akakimbia kundini na kuchukua ndama mmoja akamchinja, akampa mtumishi amwandae. Akaingia hemani, chini yake, akamwambia Sara akande unga, atengeneze kidogo, atengeneze chakula kidogo, atengeneze mkate, na atengeneze keki mekoni. Akazileta na akaandaa. Wakati alipokuwa ameketi pale, akila, walianza kuona, Mtu huyu aliendelea kuangalia upande wa Sodoma. Naye akasema . . .

70 Wawili wao, mnakumbuka, walikwenda Sodoma. Wawili walikwenda Sodoma. Tafadhali usikose hili. Ninarejea kwa kile alichosema Yesu. Wawili wao walikwenda Sodoma kumtoa Lutu na kile kilichokuwa tayari kutolewa chini kule. Halafu hao wawili ambao walishuka kwenda huko, walienda wakahubiri. (Na palikuwa na Mmoja aliyebaki na Ibrahimu, angalia ishara aliyoitenda.) Walikuwa na ishara chini kule, kulikuwa . . . Wasodoma walipigwa upofu. Kuhubiri Injili sikuzote kunampofusha asiyeamini. Na angalia alilotenda.

71 Sasa, kuna Mmoja aliyesimama nyuma kule na akatenda ishara mbele ya Ibrahimu.

72 Sasa, umewahi kutambua, mwana historia ye yote, fuatilia maandiko, fuatilia historia, hapajakuwa na wakati katika nyakati za kanisa ambapo aliondokea mtu kwenda kwenye makanisa ya kawaida nje huko katika ulimwengu, nje huko katika madhehebu, hapakuwepo mtu ambaye jina lake liliishia kama Ibrahimu, h-a-m, hapo kabla. Lakini leo wana mmoja, G-r-a-h-a-m. Hilo ni sawa. Akiwaendea huko, akiwaita watoke. Anatenda kazi ya ajabu kwa jambo hilo. Graham, Billy Granham, mtumishi wa Mungu nje huko miongoni mwa madhehebu, wanasiasa, na kadhalika, akiyapondaponda.

73 Hivi majuzi walipomtaka agombee Urais, alikataa kabisa. Mungu, mbarikie hilo. Mbona, hizo kampuni za wiski, kamwe asingalifikia hatua ya kwanza kama ingalivyokuwa. Wangetumia mabilioni ya dola, kwa sababu angezitupilia nje kwa vyo vyote, hizo kampuni za sigara na vitu kama hivyo. Unaona, yuko nje kule kama mjumbe wa Mungu kwa Wasodoma. Hilo ni kweli kabisa.

74 Lakini kumbuka, palikuwepo na Mmoja aliyebakia juu kule na Ibrahimu, Mtu mwingine, sio hao wawili ambao walishuka kwenda kule, kama wainjilisti wa kisasa ambao walishuka kwenda kule kuhubiri. Angalia, kulikuwa na Mmoja aliyebakia juu huko. Wawili walishuka wakaenda *hivi*, na Mmoja alibakia

hapa pamoja na Ibrahimu. Na huyo Mmoja ambaye alibakia na Ibrahimu alimpa ishara.

75 Sasa angalia, jina lake lilikuwa "Abramu" na mkewe alikuwa "Sarai," mnamo kama siku moja au mbili kabla ya hilo. Mungu alikwisha mtokea na kumwambia, "Ninabadilisha jina lako sasa toka Abramu liwe Ibrahimu." (Unaona, G-r-a-h-a-m ni herufi sita, binadamu.) Lakini A-b-r-a-h-a-m ni saba, herufi saba; h-a-m, huishia na h-a-m.

76 Sasa, juu hapa katika Kanisa la kiroho, palikuwepo na Mmoja juu kule kwa Ibrahimu, na angalia ambalo alisema. Alisema, "Ibrahimu," (si "Abramu") "Ibrahimu, yu wapi mkeo" (si S-a-r-a-i) "S-a-r-a? Yuko wapi Sara mkeo?"

77 Angalia alilosema, "Yumo hemani nyuma Yako."

78 Naye akasema, "Nitakurudia. Nitakurudia." Angalia hicho kijina, Yule Mmoja, kulingana na ahadi ambayo alikuwa ametoa. Huyo alikuwa Mungu! Alisema, "Nitakurudia."

79 Na Sara, (kwa namna ambayo sote tungeelewa), alicheka kimoyomoyo, moyoni mwake, alisema, "Mimi, mwanamke mzee, umri wa miaka mia moja, bwana wangu" (ambaye alikuwa Ibrahimu) "mzee pia, amepita wakati wa maisha hayo kama vijana." Akasema, "Naam, hatungeweza kuwa na furaha kama hiyo tena, mimi ni mzee na yeye ni mzee." Kisha akasema, "Tusingaliweza kuwa nayo." Na akasema, "Vipi? Mambo haya hayawezekani!"

80 Na yule—yule Mtu (Mungu katika mwili wa kibinadamu) akasema, "Mbona Sara amecheka na kutia shaka, akinena mambo haya huko hemani, nyuma?"

81 Sasa angalia, kama hiyo si huduma ile ile Yesu Kristo aliyokuwa nayo! Alitazama katika wasikizi na kutambua mawazo yao. Alimwambia Petro jina lake na jina la baba yake. Alimwambia Nathanieli.

82 Alimwambia yule mwanamke pale kisimani, wakati aliposema . . . Alisema, "Nenda uniletee maji ninywe," au "Niletee maji ninywe."

83 Akasema, "Bwana, si kawaida yenu kuzungumza na . . . ninyi Wayahudi kuzungumza na Wasamaria. Hatuna uhusiano mmoja na mwingine."

84 Akasema, "Lakini kama ungejua ni nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji." Mazungumzo yaliendelea. Akasema, "Nenda kamwite mumeo uje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Akasema, "Umesema vema, kwa maana umekuwa na watano."

Akasema, "Bwana!"

85 Angalia tofauti kati ya huyo na wao—na wao makuhani wa wakati huo, halmashauri hiyo iliyoishi katika mng'aro wa wakati mwingine. Walisema, "Huyu ni Ibilisi!" Ilibidi wawajibu kusanyiko lao kwa jambo fulani, sababu hilo lilihitajika.

86 Lakini alifanya nini maskini mwanamke huyu, Mbegu ile iliyochaguliwa hapo awali ikiwa moyoni mwake. . .Alikuwa amechefuka moyo na kuchoshwa na mambo hayo, amekwenda mitaani kama kahaba. Lakini alipoona Hilo, alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe u Nabii. Hatujawa na mmoja kwa miaka mia nne, na tunaambiwa kwamba atakapokuja Masihi hayo ndiyo mambo atakayofanya." Loo, jamani! Mara Mbegu ile iliyokuwemo mle ndani ikapata uhai! Kwa nini? Haikuhitaji tafsiri yo yote.

87 Yesu akasema, "Ni mimi ninayezungumza nawe." Hilo halikuhitaji tafsiri yo yote. Alikuwa ameishatenda muujiza na ameshuhudia kwamba Yeye alikuwa Masihi, amina, na kuthibitisha sawasawa kile Mungu aliahidi. ("Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii kama mimi," akasema Musa). Ilikuwa nini? Thibitisho la Maandiko!

88 Akakimbia kwenda mjini, na akasema, "Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Kristo? Je! huyu siye Yeye? Aliniambia niliyofanya."

89 Sasa tazama, Yesu, huyo alikuwa Yeye juu kule katika Mtu yule aliyekuwa ameuelekeza mgongo Wake hemani na akamwambia Sara alilokuwa akiwazia ndani ya hema.

90 Neno la Mungu husema, katika Waebrania, sura ya 4, kwamba. . .Anasema hili, "Neno la Mungu lina nguvu zaidi na lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, lachoma hata kugawanya viungo na mafuta yaliyomo ndani ya mfupa, na kutambua mawazo na makusudi ya moyo." Ni lile Neno! Na kila wakati ambapo nabii alikuja, alikuja na Neno, naye alikuwa Neno kwa wakati huo. Na lilitenda nini? Mtabiri aliyetambua mawazo ambayo yalikuwa katika moyo.

91 Lilitenda hilo katika Yesu Kristo kwa sababu Yeye alikuwa utimilifu wa Neno.

92 Na Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Roho wa Mungu angekuja duniani katika umbo la mwanadamu. Mungu akidhihirishwa katika mwili wa wanadamu (Amina! Unaliona hilo?), na angetenda jambo lile lile ambalo Mungu alitenda katika mwili wa kibinadamu Sodoma. Kumbuka, walikuwa wakingojea mwana wa ahadi. Na mara baada ya hilo, mwana wa ahadi alikuja. Hiyo ndiyo iliyokuwa ishara ya mwisho ambayo Sodoma na kundi la Ibrahimu waliyoona kabla ya mwana aliyeahidiwa kuja. Uliliona hilo? Na sasa Kanisa la kiroho limefikia saa hiyo.

93 Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, je! ulisema huyo alikuwa Mungu?"

94 Biblia ilisema, "Alikuwa Mungu!" Haihitaji tafsiri yo yote. Yeye ni Elohim. Hivyo ndivyo Ibrahimu alimwita. Kila msomaji wa Biblia anajua hilo. *Elohim*, "Yule ajitoshelezaye kwa yote." Alikuwa wa Kwanza, wa Mwisho; Mwanzo, Mwisho. Elohim! Ibrahimu alimwita "Elohim." Mungu (katika herufi kubwa katika Kiebrania), Elohim; kama alivyokuwa hapo mwanzo, "Mungu," Elohim.

95 Yeye alikuwa Elohim aliyedhihirishwa katika mwili wa kibinadamu, akivaa nguo za kibinadamu, akila chakula cha kibinadamu. Amina! Ishara kwamba katika siku za mwisho kwamba Mungu atatokea tena miongoni mwa watu Wake katika mwili wa kibinadamu! Amina! Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja Kwake Mwana wa Adamu." Amina! Hilo halihitaji tafsiri yo yote; linahitaji udhihirisho, hilo ndilo linalohitajika. Amina. Unaamini hilo?

Tuinamishe vichwa vyetu:

96 Baba yetu wa Mbinguni, tunakupa Wewe ahadi Yako usiku wa leo kwamba ulisema mambo haya. Uliyaahidi. Hakuna awezaye kulifanya Neno Lako liishi isipokuwa Wewe. Ulisema, "Iwe nuru," ikawa nuru. Hakuna mtu apaswaye kufasiri hilo, lilidhihirishwa.

97 Kama tulivyomnukuu Isaya, nabii, "Bikira atachukua mimba," alichukua mimba; haihitaji udhihirisho wo wote, alilitenda. Hilo ndilo lililotukia.

98 Ulisema, atakapokuja atazaliwa Bethlehemu. "Katika Bethlehemu, Yuda. Hu mdogo kamwe katika majumbe wote wa Yuda, ya Israeli? Lakini kutoka kwako atatoka Mtawala wa watu Wangu."

99 Mambo ambayo angetenda, jinsi angelia msalabani, jinsi angehukumiwa, kuchomwa miguu Yake na mikono; "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tumepona."

100 Jinsi ambavyo Daudi alisema, "Sitaacha kuzimu nafsi Yake, wala sitamuacha. . . Mtakatifu kuona uharibifu." Na siku ya tatu, kabla hayajatimia masaa sabini na mawili kuuharibu mwili Wake, Neno la Mungu lilisema, "Atafufuka." (Walisema hao waliuiba mwili Wake; bado wanaamini hilo.) Lakini tunaamini, Bwana, Neno Lako! Lilidhihirishwa. Yesu Kristo alifufuka na akasema, "Nita. . . Tazama, Mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari."

101 Na tunaamini kwamba upo hapa usiku wa leo. Tunaamini kwamba u Yesu Kristo jinsi ile ile usiku wa leo, hapa, kama ulivyowahi kuwa. Nawe unatafuta tu macho, mikono, miguu, vinywa, nafsi, miili, ambayo unaweza kutumia kujidhihirisha Mwenyewe. Mungu, tutakase usiku wa leo, ili tumwone Yesu Kristo aliye hai akiishi miongoni mwetu. Hebu na aje! Ndipo itakapokuwa, kama njaa ya wale Wayunani waliokuja siku ile, na kusema, "Bwana, twataka kumwona Yesu." Nao wakamuona. Loo, hapana shaka ilikuwa furaha kubwa sana walipomtazama!

102 Na, Mungu, Wewe u Yeye yule leo. Na uliahidi kwamba kama tukikuonea shauku tungeweza kukuona. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona" (yule asiyeamini); "lakini hata hivyo ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Tunajua kwamba Wewe u yeye yule jana, leo, na hata milele.

103 Bwana, maneno yameisha nenwa, yameisha andikwa, sasa hebu na ifanyike kwa Utukufu wa Mungu, kuonyesha kwamba hutimiza Neno Lake. Amina. Mungu awabariki.

104 Nitafanyiza mstari wa maombi. Naamini Billy alisema alitoa kadi za maombi, moja hadi mia, au kitu kama hicho. Hayupo hapa sasa hivi. Ni. . . Ni kadi ya maombi namba. . . Mtu fulani angalia nyuma yako. . . Ingekuwa—ingekuwa namba na he—na herufi (A,B,C, D au. . .). Ni nini, A? Sawa.

105 Hebu na tupate A, namba moja, mbili, tatu, nne, tano. Anza tu kusimama juu hivi. A, namba moja, namba mbili, namba tatu, namba nne. Nne, sikuiona ikisimama. Kadi ya maombi namba nne. Moja, mbili, tatu. Maombi. . . Labda hawawezi kusimama. Kama hawawezi, mtu na aangalie kadi ya mwenzako, huenda akawa na kadi na asiweze kusimama. Haraka sasa. Hiyo hapo, nne. Tano, kadi ya maombi namba tano. Sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili. Anza tu kuja hapa sasa namba yako ikiitwa. Namba moja, mbili, tatu, hebu tu njoni moja kwa moja upande huu. Kadi ya maombi namba moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, chukueni mahali penu. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano. Mtu tu ye yote ambaye hawezi. . .

106 Namwona kijana mwanamume katika gari la kusukumia wagonjwa nyuma kule. Kama namba yako inaitwa, mwanangu, na—na kama huwezi kupata. . . vema, hebu inua mkono wako tu, tutahakikisha kwamba utafika hapa. Unaona?

107 Wangapi hapa ndani hawana kadi ya maombi na bado mnaumwa? Hebu tuone mikono yenu, po pote. Papa hapa, hilo ni sawa, inueni mikono yenu juu. Mnaamini? Wakiwa wanawakusanyika pamoja, mnaamini hili, kwamba ni Yeye yule

jana, leo, na hata milele? Wangapi? Angalia hawa wahudumu; hivi maandiko hayaneni kwamba leo, ndugu zanguni, kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu ambaye angeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu? Hilo ni sawa? Wangapi wanaamini hilo, inua mkono wako? Yeye ni Kuhani Mkuu ambaye anaweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu.

108 Basi kama Biblia inasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," wangapi wanaamini hilo? Basi atatendaje leo? Itampasa kutenda kama alivyotenda jana. Sivyo? Usiku wa leo Yeye yuko wapi? Ameketi katika mkono wa kuume wa Ukuu, mwili Wake; Roho Mtakatifu yuko hapa katika jengo, kumjulisha.

109 Angalia, sasa tazama. Kulitukia nini wakati mtu fulani alipomgusa vazi Lake nyuma kule, mwanamke siku moja? Hakuwa na kadi ya maombi, tungesema, lakini aligusa vazi Lake. Na alipogusa vazi Lake, Yesu aligeuka na akasema, "Nani amenigusa?"

110 Petro alimkemea, akasema, "Vipi, Bwana, hilo halionekani kuwa jambo la hekima. Naam, kila mtu anajaribu kukugusa. Kwa nini useme, 'Nani amenigusa?'"

111 Akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa mdhaifu." Wangapi wanajua hilo? *Uweza,* ambalo humaanisha "nguvu," zilimtoka. "Nimekuwa mdhaifu, mtu fulani alinigusa na mguso wa namna nyingine." Naye akageuka na kuangalia katika kusanyiko mpaka alipopata ambapo imani ile ilikotokea.

112 Kila mmoja alikuwa akimkumbatia, "Ee Rabi, tunakuamini," na yote haya.

113 Lakini palikuwepo na mtu fulani aliyeamini hasa Jambo hilo. Naye akagusa vazi Lake kisha akaamini kwamba ameponywa, kwa sababu alisema moyoni mwake kama angeweza kulitenda hilo hilo ndilo lingetukia.

114 Aligeuka na akaliangalia kusanyiko mpaka akampata, akasema . . . akamwambia kutokwa kwake na damu kumeisha koma naye amepona. Sivyo? Sasa, hivyo ndivyo alivyofanya katika kusanyiko la watu.

115 Sasa, ninadai kwamba hajakufa, Yu hai leo kama alivyokuwa daima. Na Biblia alisema, Yesu alisema, Mwenyewe, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu."

116 Sasa tazama, hata Mungu awe na kipawa cha namna gani juu hapa, yabidi kuwe na mtu chini kule, pia, kukiitikia. Yeye alikwenda katika mji, Biblia ilisema, "Kulikuwa na mambo mengi asiyoweza kutenda kwa sababu ya kutokuamini kwao." Sivyo? Kitu kile kile leo. Yakupasa umwamini. Yakupasa tu kumwamini. Hiyo ndiyo njia pekee unayoweza.

117 Msitari wa maombi uko tayari? Sasa kila mmoja awe na kicho kwa kama dakika kumi tu. Sijui kama nitaweza kupita

hapo, ninao kama ishirini na watano au thelathini wanasimama pale. Lakini sasa, katika mstari wa maombi, kila mmoja wenu nje huko katika mstari wa maombi anayejua kwamba mimi ni mgeni kwenu, nami sijui cho chote kukuhusu, inua mkono wako. Kila mmoja katika mstari wa maombi.

118 Sasa kule nje katika kusanyiko, ambao mnajua sijui kitu cho chote kuwahusu ninyi, inua mkono wako. Unaona? Sasa, sasa, hili hapa ambalo ninajaribu kusema, rafiki, unaona. Sasa liko hapa. Wahudumu wote hawa hapa jukwaaani . . . Na Kristo alitoa ahadi hii. Unaona, imeandikwa. Lingetimia lini? Katika siku za mwisho, kabla tu ya kule Kuja kwa Bwana. Sivyo? Lilipaswa kutimia wakati huo.

119 Sasa, hilo ndilo Neno lililotabiriwa leo. Si nuru ya Luther; si nuru ya Wesley; na hata si nuru ya Kipentekoste. Ipo inawaka, inawaka barabarani sasa. Sasa, Luther ni sawa; Methodisti ni sawa; Batisti ni sawa; wote, Upentekoste, ni mzuri. Wapo wa kila aina wameketi hapa usiku wa leo. Sio—sio—sio watu mmoja mmoja. Je! Vipi kama yule . . .

120 Usingeweza kumwambia Mmethodisti kitu cho chote kuhusu Luther, kwa sababu anaamini katika utakaso na Luther haamini. Unaona?

121 Kamwe huwezi ukamwambia Mpentekoste kwamba “utakaso umetosha,” ameona kurudishwa kwa vipawa. Hataamini hilo. La, ana cha zaidi ya hayo. Unaona? Na huo ni wakati wa mwisho wa kanisa tuliokuwa nao, na Biblia husema hakutakuwa na nyakati zingine za kanisa tena.

122 Lakini kuna kukusanyika kwa watu, unaona, nasi tupo hapa. Sasa, kumbuka, ile ishara ya mwisho. Je! Sisi watu tunangojea mwana wa ahadi? Inua mkono wako. Mnaamini mu Wazao wa Ibrahimu kwa kuwa katika Kristo? Inua mkono wako. Basi, enyi Wazao wa Ibrahimu, pokeeni ishara yenu! Haipo kule nje Babeli, haipo kule nje katika ulimwengu wa kidhehebu. Ipo hapa miongoni mwenu, ninyi ambao hammo katika ile fujo nje huko. Iaminini!

123 Hapa yupo mwanamke, ni mgeni kabisa kwangu, tuna karibu umri mmoja. Sijawahi kumwona mwanamke huyu maishani mwangu. Kama ningeweza kumponya mwanamke huyo ningelitenda hilo, kama yu mgonjwa. Sijui kitu kumhusu yeye. Ulimwona akiinua mkono wake dakika chache zilizopita. Kamwe si—sijamwona. Yeye ni mwanamke tu anayesimama pale.

124 Leo wameshuka wakaja hapa na kuleta kadi kadhaa za maombi, wakazichanganya na kuwapa watu. Mmoja alipata namba moja hapa, na namba kumi nyuma kule, namba kumi na tano, namba saba, namba . . . namna hiyo tu. Zote zimechanganywa, mbele yenu kabisa, kila siku. Na wakati zinapoitwa, zinaitwa tu kila mahali kutoka kila mahali. Unaona?

Na, sasa, si lazima uwe na kadi ya maombi, keti tu hapo na uamini. Kwa nini hamwezi . . .

125 Jifinye mwenyewe, usiku wa leo, chunguza saa ile tunayoishi. Unaona? Sasa, imekaribia sana kwisha, pia, rafiki. Karibu sana kwisha!

126 Sasa, kama Mungu wa Ibrahimu alimfufua Yesu Kristo kutoka kwa wafu, na kwamba Yesu aliahidi kwamba katika siku za mwisho ishara zile zile ambazo Ibrahimu . . . kwamba Malaika yule (ambaye alikuwa Mungu katika mwili wa kibinadamu) alitenda mbele ya Ibrahimu, kabla tu ya mwana aliyeahidiwa kutokea, Yesu alisema kitu kile kile kitatendeka leo.

127 Sasa, tunaona atomiki na madhehebu, na yote hayo, na mchafuko waliomo ndani yake. Tunamuona Billy Graham chini kule, na Oral Roberts, na watu hao wote nje huko; mjumbe wa Kipentekoste na mjumbe wa kidhehebu chini kule, tunaona yote hayo yakiendelea, ile ishara ikitendwa. Billy Graham, mwanatheolojia kwelikweli, ambayo dhehebu kuamini. Oral Roberts, mponyaji kweli kweli, hasa, sawa kabisa na Pentekoste.

128 Lakini tazama hapa, kuna kitu kingine kilichoahidiwa kwa Mzao wa Ibrahimu. Wao wako huko chini miongoni mwa madhehebu; kuna kitu *nje* ya madhehebu kinachopaswa kutukia, kuwakusanya watu. Tutaliacha lipite hadi kesho usiku.

129 Tazama, simjui mwanamke yule. Nitampa kisogo. Kama Bwana atanena kitu kwa mwanamke huyo, labda ni—ni mambo ya kinyumbani, labda ni mambo ya kifedha, labda ni ugonjwa; sijui. Atajua kama ni ukweli au la.

130 Kama atatenda jambo lile lile usiku wa leo ambalo alitenda wakati huo, utamwamini Mungu yule ambaye Yesu Kristo aliahidi atakuwa hapa katika siku za mwisho? Wangapi wanaamini kwamba tunaishi kama katika Sodoma, wakati ulimwengu wote umeingia katika hali ya Kisodoma? Wangapi wenu mnaamini kwamba niliyowaambia usiku wa leo ni Kweli? Basi enyi watoto na Wazao wa Ibrahimu, muaminini Mungu!

131 Hilo ni kusudi iondoe mawazoni mwenu kwamba ninajaribu kumwambia jambo fulani yule mwanamke, nikimwangalia usoni, au kuchukua mambo yote kuhusu uwezo wa kushirikiana mawazo au lo lote unalotaka kujua. Mtu ye yote ambaye anajua kuhusu uwezo wa kushirikiana mawazo angepaswa kufahamu vyema zaidi. Unaona? Unaona? Uliwahi kumuona mtu anayeshirikiana mawazo akihubiri Injili? Uliwahi kumuona muongea na mizimu akihubiri Injili, akitenda ishara na maajabu, akimtangaza Yesu Kristo vivyo hivyo? La.

132 Unaona, ni tu . . . ni akili za watu. Unaona, wao ni vipofu. Unaamini wanaweza kuwa vipofu? Biblia ilisema wangekuwa hivyo. Hilo ni sawa? "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu,

wasingiziaji, wasiojizuia, wasiopenda mema, wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake."

133 Je Yesu hakusema, katika Mt. Mathayo 24:24, kwamba "Hizo roho mbili katika siku za mwisho karibu zingewapoteza walio Wateule, kama yamkini"? Lakini haiwezekani. Walikuwa katika mawazo ya Mungu hapo mwanzo, na wao ni sehemu ya Mungu.

134 Sasa, Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, hebu na ijulikane usiku wa leo kwamba ninasema Ukweli kukuhusu Wewe. Ni Wewe, Bwana. Kwa unyenyekevu wajalie watumishi Wako kutoa mawazo yao njiani, kusudi upate kuitumia miili yetu kwa Utukufu Wako. Katika Jina la Yesu, Mwana wa Mungu. Amina.

135 Kipawa ni nini? Si kitu fulani unachochukua na kukatakata na kugeuza. La, la. Ni kujua jinsi ya kujiondoa wewe mwenyewe njiani ili Mungu apate kukutumia. Kipawa ni kujiondoa tu wewe mwenyewe, ndipo Mungu anakitumia.

136 Bibi aliye nyuma yangu atakufa mara moja kama haponywi. Bibi aliye nyuma yangu ndio karibuni tu aombewe na mtu mwingine, hivi karibuni. Ana kansa. Hiyo kansa iko katika titi lake na pia katika mapafu yake. Na yeye ndio hivi karibuni tu ameombewa, na anajaribu kulikubali kwa imani kwamba ameponywa. Hilo ni BWANA ASEMA HIVI! Hilo ni kweli, bibi? [Yule bibi anasema, "Ndio, ni kweli."—Mh.] Kama ndivyo ilivyo, wapungie—wapungie kusanyiko mkono wako. Mungu wa Ibrahimu bado anaishi! Sawa, nenda uamini unaloamini na utapona. Amina.

Unaamini? Unasema, "Vipi katika kusanyiko?"

137 Mwanamke huyu anayeketi hapa na mwenye . . . mwisho wa safu, bibi wa pili papo hapo. Nilipogeuka tu hapo niliona kitu fulani, kitu kuzunguka mkono wake, musukumo wa damu ikisukuma. Ana msukumo mkubwa wa damu. Hilo ni sawa, bibi? Inua mkono wako. Kama unaamini msukumo wako wa damu utashuka. Mungu wa Ibrahimu bado anajitokeza. Yuko tu jinsi ilivyokuwa, Neno la Mungu kwa siku hii!

138 U hali gani? Unaamini sasa? Uwe na imani katika Mungu! Ilionekana kuwa mtoto tu. Mungu anaujua moyo wako, bibi mdogo, mimi sijui. Unaamini Mungu anaweza kunifunulia kuna shida gani? Utamwamini Yeye kama nikifanya hivyo? Si kwa ajili yako, ni kwa ajili ya mtu mwingine, naye ni kaka yako. Naye ni mgonjwa sana na yuko katika jiji fulani kaskazini hapa, Tulare. Na yuko hospitalini, naye ana ugonjwa wa leukemia, na madaktari wamemkatia tamaa wakamwacha afe. Hakuna matumaini kamwe. Hilo ni kweli. Unaamini? [Yule bibi, huku analia, anajibu "Ndio."—Mh.] Sawa. Umeshika nini mkononi mwako? Chukua hicho ukamwekelee. Na usitie shaka. Amini! Amina.

139 Unaamini? Kamwe sijamuona huyo bibi maishani mwangu. Lakini Mungu yuangali Mungu! Sasa, niambie mwanadamu anayeweza kufanya hilo? Si katika maumbile ya mwanadamu kulitenda. Ni yule Mungu ambaye Yesu Kristo aliahidi atakuwa hapa katika siku za mwisho naye angejithibitisha Mwenyewe (mbele tu ya Uzao wa Ibrahimu) kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.

140 Sasa hapa, simjui huyu bibi, tu wageni mmoja kwa mwingine, ninabuni ni wakati wetu wa kwanza kukutana maishani mwetu. Unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? Unaamini hili kuwa Neno? Na unajua kwamba kama. . . Neno hili bado hutambua mawazo na makusudi ya moyo. Sivyo? Neno ni Mponya, pia, kama unaweza kuliamini. Unaamini? Wewe umefunikwa na kivuli, pia, na kivuli cheusi. Ni kansa. Na unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia kansa hiyo iko wapi? Iko katika chango, ndivyo asemavyo daktari. Unaamini sasa kwamba utaponywa? Nenda, na usitie shaka kamwe, na Mungu atakuponya. Amina.

141 Mnaamini kila mtu? Sawa tu kabisa na alivyoahidi kutenda! Mwaminini Mungu, msitie shaka.

142 Tu wageni mmoja kwa mwingine. Mimi sikujui. Kama hatufahamiani, hebu kusanyiko lijue hilo, tunashikana mikono yetu. Sijamuona huyu mwanamke maishani mwangu.

143 Mnaamini ninyi mlioko huko? Mnaamini ni Yesu Kristo? Ni nini? Ni Neno Lake. Wakati watu hawa wanapolikataa, hawamkatai mwanadamu, wanalikataa Neno. Neno ndilo lililokuwa nje, halikuweza kurudi ndani.

144 Sasa, huyu bibi ni mgeni kwangu. Sijamwona maishani mwangu. Mungu ni Mponya. Inaweza isiwe ni kwa ajili ya uponyo, yaweza iwe ni kwa ajili ya jambo lingine, lakini kama Mungu atanieleza shida yako ni nini, je, utaniamini? Jambo la kwanza unalotakia maombi, ni, una sikio bovu. Moja ya masikio yako, huwezi kusikia kwalo. Hiyo ni sawa. Hiyo ni kweli. Na halafu una tabia fulani, nawe unataka kuondoa tabia hiyo, ni kuvuta sigara. Weka kidole chako katika sikio lako zuri sasa, vema, sikio lako zuri. Vema. Sasa mwamini Mungu na ushike njia uende, na usi. . . na wala hutavuta sigara tena kama utaamini. Nenda zako, na Bwana akubariki.

Unaona kilichotukia. Je! si Yeye ni halisi?

145 Sikujui, tu wageni mmoja kwa mwenzake. Sijakuona kamwe maishani mwangu, lakini Mungu anakujua. Kama Mungu anaweza kuniambia kitu fulani kukuhusu, utaamini?

146 Kusanyiko lote litaamini? Mtu ye yote nje huko anamjua huyo mwanamke? Kuna mtu ye yote katika kusanyiko hili anayemjua huyo mwanamke? Vema, mnajua kama hili ni kweli au la. Hili lingemaliza hilo, hili lingesema ukweli.

147 Sasa waweza kuona lililotukia katika dakika chache zilizopita, unaona, ni kwamba tu ninapepesuka, unaona, ni kwamba tu ninakuwa kipofu kwa kila kitu. Unaona, ni kutambua. Unaona, ni Roho Mtakatifu, si mimi. Ni Neno lililoahidiwa kwa siku hii! Haijatendeka tangu siku za mitume, haijatendeka. Lakini mahali iliponenwa, "Katika kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu. Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Mwana wa Adamu." Wasioamini hawaliamini, hawakusudiwi kuliamini. Lakini waamini wanaliamini!

148 Sasa, kama Roho Mtakatifu atafunua hili, wangapi wataamini kwa mioyo yenu yote, mtainua mikono yenu?

149 Umeumia. Umepata ajali ya motokaa, imetengua baadhi ya mifupa katika shingo lako. Pia una figo iliyosogea. Hiyo ni kweli, siyo? Unaamini? Utakuwa mzima. Bwana asifiwe.

150 Unaamini Mungu huponya shida ya figo? Basi nenda zako na ukubali uponyo wako.

151 Njoo ewe bibi. Tazama huku. Unaamini Mungu huponya shida ya moyo? Vema, nenda zako na uamini, na moyo wako utapona.

152 Njoo hapa. Unaamini Mungu anaweza kukuponya mgongo wako, kukufanya mzima? Endelea na uamini hilo basi.

Mwamini Mungu tu, hayo ndiyo tu yakupasayo kutenda!

153 Njoo bibi. Unaamini mungu anaponya shida ya tumbo? Nenda, ukale chakula chako cha jioni, amini kwa moyo wako wote.

154 Njoo. Unaamini Mungu anaweza kuponya yabisi kavu? Basi nenda zako, amini, na aku . . . na Mungu atakuponya.

155 Vema, njoo. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini? Yabisi kavu, tena. Unaamini Mungu anaweza kukuponya? Nenda zako, amini hilo, useme, "Asante, Bwana."

Wangapi wanaamini nje huko? Mnaamini?

156 Bibi huyu aliyeketi hapa amevaa nguo nyekundu, akiinua mkono wake papa hapa, akiugua msukumo wa damu. Unaamini Mungu anaweza kukufanya mzima? Unaamini? Vema. Weka mikono yako juu ya bibi yule anayekufuatia chini kule, na umwambie sauti yake itakuwa sawa. Amina.

Hilo hapo. Amina. Unaamini? Uwe na imani!

157 Hapa yuko mtu ameketi hapa, ana ugonjwa wa kuvunja na damu. Unaamini, bwana, unayeketi papa hapa? Ndio, una ugonjwa wa kuvunja damu. Unaamini utapona?

158 Bibi anayekufuatia ana ugonjwa wa kuvunja damu pia, na ana shida ya mgongo. Unaamini Mungu atakuponya? Unaamini? Inua mkono wako na ulikubali. Amini.

159 Bibi huyu anayekufuatia ana matatizo kwenye miguu yake na nyonga yake. Unaamini kwamba Hilo ni sawa, bibi? Unaamini kwamba utaponywa? Vema, inua mkono wako, useme, “Ninaukubali.”

160 Vema, bibi anayemfuatia anao ugonjwa wa kuambukiza. Unaamini kwamba Mungu ataponya ugonjwa huo wa kuambukiza, bibi kijana mwenye miwani? Inua mkono wako, sema, “Naukubali.” Vema, amini hilo.

161 Bibi anayemfuatia ana shida ya figo. Unaamini Mungu atakuponya hiyo shida ya figo, bibi? Vema, inua mkono wako, likubali.

162 Msichana mdogo anayemfuatia ana tezi. Unaamini Mungu ataponya tezi hiyo hapo? Inua mkono wako, likubali.

163 Wangapi mnaamini kwa mioyo yenu yote? Basi simameni kwa miguu yenu mkalikubali. Simameni katika uwepo wa Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Yakobo.

164 Katika Jina la Yesu Kristo Roho Mtakatifu na ashuke humu jengoni sasa na kumponya kila mtu aliyepo katika Uwepo wa Kiungu!

MUNGU NDIYE ANAYEJIFASIRIA SWA64-0205
(God Is His Own Interpreter)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, Februari 5, 1964, katika Kern County Fairgrounds kule Bakersfield, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org